JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

Kumb.Na. **EB.32/160/01/209**

**28 Februari, 2025**

Mkurugenzi Mtendaji,
Pasua Media Limited,
T/A Pasua FM Radio,
S.L.P 8016,
**DODOMA.**

**UAMUZI JUU YA AMRI YA UTEKELEZAJI**

*(Kwa mujibu wa Amri ya Utekelezaji iliyotolewa kwa Pasua Media Limited ya tarehe 25 Septemba, 2024)*

**1. UTANGULIZI**

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (inayorejewa hapa kama **"TCRA**"), mnamo tarehe 21 Mei 2020 ilitoa leseni ya huduma za Utangazaji wa Redio ya Kibiashara (inayorejewa hapa kama **"Leseni"**) na kutoa Masafa ya Redio kwa Pasua Media Limited, T/A Pasua FM Radio, (inayorejewa hapa kama "**Mtoa Huduma**") kwa ajili ya utoaji wa huduma za utangazaji wa Redio.

1.2 Leseni iliyotolewa kwa Mtoa Huduma inamtaka, pamoja na mambo mengine, kuzingatia sheria, kanuni na masharti ya Leseni.

1.3 Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, [Sura ya 306], kikisomwa pamoja na Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Leseni), 2018, kinamtaka Mtoa Huduma kulipa ada za Leseni kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni.

1.4 Kifungu cha 21(h) Sura ya 306 kinaeleza kuwa kurudia kutokulipa ada kwa Mtoa Huduma, kama inavyotakiwa kisheria, ni ukiukwaji mkubwa unaoweza kusababisha kusitishwa au kufutwa kwa Leseni chini ya kifungu cha 22(a), Sura ya 306.

1.5 Kumbukumbu za TCRA zinaonyesha kuwa, licha ya Mtoa Huduma kukumbushwa mara kadhaa na TCRA, ameendelea kutoa huduma bila ya kulipa ada za leseni kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi na Tatu Laki Tisa Sabini na Tisa Elfu Mia Tatu Sitini (TZS. 13,979,360).

## 2. AMRI YA UTEKELEZAJI

Mnamo tarehe 03 Oktoba 2024, TCRA ilitoa amri ya utekelezaji kwa Mtoa Huduma ikimtaka kuwasilisha utetezi wa kimaandishi na kufika mbele ya TCRA tarehe 21 Oktoba, 2024 saa 4:00 asubuhi kujieleza kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria kwa kushindwa kulipa ada za leseni kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi na Tatu Laki Tisa Sabini na Tisa Elfu Mia Tatu Sitini (TZS. 13,979,360) kinyume na kifungu cha 15(1) Sura ya 306 na Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Leseni), 2018.

## 3. KUSIKILIZWA KWA UTETEZI

3.1 Mtoa Huduma aliwasilisha utetezi wake wa kimaandishi na kufika TCRA tarehe 21 Oktoba 2024 saa 4:00 kuwasilisha utetezi wao wakiwakilishwa na Bw. Erick Cyprian David, ambaye ni Mkurugenzi wa Mtoa Huduma. Katika utetezi wake, Mtoa Huduma aliwasilisha yafuatayo:

3.1.1 Mtoa Huduma alikiri kushindwa kulipa ada ya leseni kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi na Tatu Laki Tisa Sabini na Tisa Elfu Mia Tatu Sitini (13,979,360);

3.1.2 Aliendea kueleza kuwa kutokulipa ada za Leseni kulitokana na sababu mbali mbali, ikiwemo kuunguliwa na mitambo ya utangazaji wa Redio, hali iliyopelekea kununua vifaa vingine.

3.1.3 Vilevile, alielekeza lawama zake kwenye ukosefu wa matangazo ya kutosha kwenye soko, kwani matangazo ndio chanzo kikuu cha mapato ya Redio na kinategemewa kwa ajili ya kuendesha Redio pamoja na kulipa kodi na ada mbalimbali;

3.1.4 Mtoa Huduma alidai kwamba, ili kupambana na hali ya changamoto ya fedha za kuendeshea kituo cha Redio, wameanzisha vyanzo vipya vya mapato ambavyo vinajumuisha uanzishaji wa kiwanda cha sabuni, mikopo kutoka kwenye mfuko wa Vision Fund, pamoja na gari la matangazo la bidhaa mbalimbali ili kufanya maonyesho barabarani ambayo yatakuwa ni chanzo mbadala cha mapato;

3.1.5 Aidha, Mtoa Huduma pia aliieleza TCRA kuwa, wanatarajia kupata mapato kutokana na huduma za matangazo walizotoa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambazo wanatarajia kulipwa mwezi Novemba, 2024. Alieleza kuwa, hatua zote zilizochukuliwa zina lengo la kusaidia kukusanya mapato ya kituo ili kutimiza wajibu wake wa kulipa ada ya Leseni na Masafa;

3.1.6 Mtoa Huduma aliahidi kuwa tarehe 22 Novemba, 2024 atalipa robo ya deni wanalodaiwa na TCRA na mwisho wa mwezi Novemba, 2024 kuendelea na malipo kwa awamu ya Shilingi za Kitanzania Milioni Moja na Laki Tano (TZS. 1,500,000) na kuendelea kulipa kwa miezi sita ambapo anaamini atakamilisha deni lote ifikapo mwezi Aprili, 2025.

3.1.7 Alihitimisha kwa kuiomba TCRA isifute leseni ya Pasua Media Limited kwa kuwa:

(i) Pasua Media Limited inamilikiwa na kijana wa Kitanzania ambaye anatazamwa na kundi kubwa la vijana kama mfano na motisha kwao. Hivyo basi, kusimamishwa au kufutwa kwa Leseni ya Mtoa Huduma kutakuwa na athari hasi kwa vijana.

(ii) Kituo cha Redio cha Pasua Media kinafanya kazi ya kuendeleza vijana kwenye tasnia ya habari kwa kupokea vijana wengi wanaofanya mafunzo kwa vitendo. Kwa kufanya hivyo kituo kimekuwa kikiongeza tija kwenye tasnia ya habari na hivyo kuchangia maendeleo ya jamii.

(iii) Kwamba Mtoa Huduma ana imani ya kumaliza deni hilo ndani ya muda alioahidi na kwamba hatorudia tena kulimbikiza ada za leseni.

## 4 UZINGATIAJI WA UTETEZI

Baada ya kuzingatia utetezi wa Mtoa Huduma aliowasilisha kwa maandishi na kwa mdomo, TCRA imezingatia utetezi huo kama ifuatavyo:

4.1 Kukiri kwa Mtoa Huduma kushindwa mara kadhaa kulipa ada za Leseni kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi na Tatu Laki Tisa Sabini na Tisa Elfu Mia Tatu Sitini (TSH. 13,979,360).

4.2 Kuhusu utetezi wa Mtoa Huduma kuwa kutolipa ada za Leseni kumetokana na sababu mbali mbali ikiwemo kuungua kwa mitambo, TCRA imeshindwa kushawishika na hoja hii kutokana na kuwa kumbukumbu zinaonesha kwamba Mtoa Huduma amekuwa na tabia ya kutolipa ada tangu alipopatiwa leseni. Kwa mfano:

(i) Tarehe 17 Septemba 2021 Mtoa Huduma alipewa Notisi ya ukiukaji wa masharti ya Leseni (*Notice of Material Breach*) kwa kushindwa kulipa ada ya Leseni na Masafa zinazofikia TZS 5,091,700 na kupewa siku thelathini (30) kulipa deni husika, notisi ambayo haikuzingatiwa wala kutekelezwa;

(ii) Tarehe 27 Januari 2022, TCRA ilimkumbusha Mtoa Huduma kwa mara nyingine kulipa ada ya Leseni lakini bado mtoa huduma hakutekeleza;

(iii) Tarehe 13 Julai 2023, TCRA ilitoa Amri kwa Mtoa Huduma kusimamisha utoaji wa huduma za utangazaji kutokana na kushindwa kulipa ada za Leseni zilizokuwa zimefikia TZS 15,529,360;

(iv) Tarehe 8 Februari 2024, Mtoa Huduma aliahidi kulipa ada anazodaiwa kwa awamu na kumaliza madeni yote ifikapo tarehe 28 Septemba 2024. Hata hivyo, hakutekeleza.

4.3 Kushindwa kwa Mtoa Huduma kulipa ada za Leseni na kushindwa kutimiza ahadi alizojiwekea mwenyewe kumaliza deni kunaonesha jinsi Mtoa Huduma alivyo mkiukaji wa kudumu wa sharia na masharti ya leseni. Hali hii inatoa ishara kuwa, kituo hiki cha redio kimeshindwa kujiendesha na hakuna jitihada dhahiri za kulipa madeni ambayo yameshalimbikizwa na kuendelea kutoa huduma bila ya madeni.

4.4 Kuhusu pendekezo jipya juu ya namna ya kulipa ada za leseni zinazodaiwa, pendekezo hili linatia shaka kwa Mtoa Huduma kuaminika tena na TCRA. Aidha, jambo la msingi kwa sasa ni kwa Mtoa Huduma kulipa ada zake zote za leseni, na si kutoa ahadi tena kwa kuwa ahadi kama hizo alishazitoa hapo awali na hakuzitekeleza.

4.5 TCRA haina neno juu ya vyanzo vipya vya mapato ambavyo Mtoa Huduma ameviainisha katika utetezi wake. Jambo la msingi ni kwa Mtoa Huduma kulipa ada za leseni.

4.6 Kuhusu ombi la Mtoa Huduma kutokuchuliwa hatua, kwa kuwa Pasua inamilikiwa na Kijana wa Kitanzania na ambaye anatazamwa na kundi kubwa la vijana wanaomtazama kama kielelezo na motisha kwa vijana, TCRA inapenda kufafanua kwamba uwajibikaji katika kutekeleza masharti ya leseni na sheria havihusiani kwa namna yoyote na umiliki wa kituo cha redio na mtazamo wa jamii kwa jamii hiyo. Ni vizuri kwa mtu kufanya jambo linalowatia motisha vijana au jamii inayomzunguka na kumwangalia kama mfano wa kuigwa, lakini mtazamo huo chanya unakamilika si tu kwa kuendesha kituo, ila kwa kufuata na kuzingatia sharia na masharti ya Leseni.

4.7 Aidha, Mamlaka inatambua kuwa baada ya kuitwa kutoa maelezo kwa mujibu wa Amri ya Utekelezaji, Mtoa Huduma amelipa sehemu ya deni kwa kiasi cha Shilingi Milioni Tano Laki Tisa Tisini na Moja na Mia Saba (TSH 5,991,700) na kubakiza kiasi cha Shillingi Milioni Saba Laki Tisa Themanini na Saba Elf Mia Sita Sitini (TSH 7,987,660) kikiwa hakijalipwa.

## 5 UAMUZI

5.1 Baada ya Mtoa Huduma kukiri kudaiwa ada za Leseni na:

5.2 baada ya kusikiliza na kuchambua utetezi wa Mtoa Huduma, TCRA imejiridhisha pasi na shaka kwamba Mtoa Huduma ameshindwa kulipa ada za Leseni kinyume na sheria na masharti ya leseni;

**HIVYO BASI** kwa mujibu wa Kifungu 114 na 22(a) cha Sheria ya Mawasiliano na Kieloctroniki na Posta [Sura ya 306], pamoja na Kifungu 48 (2) na (3) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania [Sura ya 172], TCRA **INAIAMURU** Pasua Media Limited T/A Pasua FM Radio:

1) Kulipa, ndani ya siku sitini (60) tangu tarehe ya uamuzi huu, kiasi cha Shilingi Milioni Saba Laki Tisa Themanini na Saba Elfu Mia Sita Sitini (TSH 7,987,660); na
2) Iwapo Pasua Media Limited T/A Pasua FM Radio itashindwa kutekeleza amri hii Leseni iliyotolewa kwa Pasua Media Limited T/A Pasua FM Radio itasitishwa.

**TAMBUA KUWA** endapo Pasua Media Limited itashindwa, kukataa, kupuuza au kutokutii amri hii, TCRA itaendelea kuchukua hatua zaidi za kisheria na za kiudhibiti inayoweza kuwa ni kuamuriwa kusitisha utoaji huduma, au kufuta leseni, kunyang'anya Masafa na kukusanya deni la ada isiyolipwa kwa mujibu wa sheria.

Uamuzi huu umetolewa tarehe...28... mwezi wa Februari, 2025.

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Fri Feb 28 22:59:02 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Uamuzi huu umepokelewa na **Pasua Media Limited T/A Pasua FM Radio** tarehe ......... mwezi wa Machi, 2025.

Jina...ERIC CYPRIAN DAVID...

Saini .................................. (Muhuri wa Ofisi)

Cheo/Wadhifa...CEO...

PASUA MEDIA LTD
P.O.Box 356
DODOMA
DAR ES SALAAM

*(Uamuzi huu umetolewa katika nakala mbili (duplicate). Tafadhali weka saini katika nakala zote mbili na ubaki na nakala yako, kisha wasilisha nakala nyingine TCRA kuthibitisha kupokea Uamuzi.)*